

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**  
ISO 9001:2015 CERTIFIED



## TAARIFA KWA UMMA

### KUTOA TAARIFA JUU YA MATUMIZI YA HUDUMA YA MTANDAO BINAFSI (VIRTUAL PRIVATE NETWORK - VPN)

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya Mwaka 2003, kwa lengo la kusimamia Sekta ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta nchini Tanzania.

**KWA KUZINGATIA** Kanuni ya 16(2) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020; mtu hatatoa, hatamiliki au hatasambaza teknolojia, programu, programu tumizi au kitu chochote kinachoendana na ambacho kinaruhusu au kumsaidia mtumiaji kupata maudhui yaliyokatazwa; na

**KWA KUZINGATIA** Kanuni ya 19(b) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui Mtandaoni za mwaka 2020; katika utekelezaji wa majukumu yake ya udhibiti wa maudhui mtandaoni, TCRA ina mamlaka ya kuchukua hatua dhidi ya ukiukaji wa Kanuni ikiwemo kuzuia upatikanaji wa maudhui yaliyokatazwa; na

**KWA KUWA**, TCRA imebaini upatikanaji wa maudhui yaliyokatazwa kwa kupitia matumizi ya mtandao binafsi (VPN) kinyume cha Kanuni;

**HIVYO BASI**, TCRA inautaarifu Umma kwa ujumla, watu binafsi na makampuni ambayo kwa asili ya majukumu na kazi zao, matumizi ya mtandao binafsi (VPN) hayazuiliki, kutoa taarifa kwa TCRA juu ya VPN wanazotumia na taarifa zote muhimu ikiwemo anuani ya itifaki ya mtandao (IP Address) kabla au mnamo tarehe 30 Oktoba, 2023 kupitia <https://www.tcra.go.tz/vpn-details-form>.

TCRA itaendelea kuchukua hatua za kiudhibiti dhidi ya matumizi ya mtandao binafsi (VPN) yasiyo halali ikiwemo kuzuia upatikanaji wa VPN ambazo hazijatolewa taarifa au kusajiliwa.

TCRA inapenda kuukumbusha Umma kuwa, utoaji, umiliki au usambazaji wa teknolojia, programu, programu tumizi au kitu chochote kinachoendana na ambacho kinaruhusu au kumsaidia mtumiaji kupata maudhui yaliyokatazwa ni kosa la jinai, linaloadhibiwa baada ya kutiwa hatiani, kwa faini ya shilingi za Kitanzania zisizopungua milioni tano au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

**IMETOLEWA NA**  
Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,  
20 Barabara ya Sam Nujoma,  
S. L. P 474,  
**14414 DAR ES SALAAM.**  
Simu: +255 22 241 2011-2  
Nukushi: +255 22 2412009  
Barua pepe: [dg@tcra.go.tz](mailto:dg@tcra.go.tz)